

Afisa Tawala wa Wilaya ya Morogoro, Bi. Janeth Chatta amewataka wananchi wa mkoa wa Morogoro kutoona fahari kwa kuwa na idadi kubwa ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika badala yake watumie fursa ya elimu ya watu wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, inayotolewa kupitia MEMKWA, MWESKWA, MUKEJA, SEQUIP na Elimu ya Ufundi, kutimiza azma ya Serikali ya kuwa na jamii ya watu walioelimika huku akiwasisitiza watendaji wa Sekta ya Elimu Mkoa wa Morogoro kuendelea kusimamia vyema elimu ya watu wazima ndani ya Mkoa.



Bi. Chatta ameyasema hayo leo tarehe 05.10.2023 alipomwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Morogoro katika maadhimisho ya kilele cha Juma la Elimu ya Watu Wazima yaliyofanyika katika uwanja wa stendi ya zamani ya daladala mjini Morogoro na kuhudhuriwa na Taasisi mbalimbali zinazotoa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ndani ya Manispaa ya Morogoro pamoja na wananchi.

“Elimu ya Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi inatolewa ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na elimu, ujuzi na maarifa ya kuwezesha kuwa sehemu ya mfumo wa dunia ambao umejikita katika Ufahamu, Maarifa na Taarifa hivyo mbali ya kutumia fursa hii, inabidi wazazi, walezi na wadau wote wa elimu mhakikishe watoto wenye umri wa kuwa kwenye mfumo rasmi wa elimu wanapata elimu” alifafanua Bi. Chatta.



Awali kabla ya hotuba ya mgeni rasmi, Afisa Elimu ya Watu Wazima wa Manispaa ya Morogoro, ndugu David Malimbwi ametaja uhaba wa walimu, vyumba vya madarasa, uhaba wa muda wa kutekeleza kwa ufanisi Elimu ya Watu Wazima, uhaba wa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wanaofundisha Elimu ya Watu Wazima, uhaba wa fedha na ulegevu wa kuifanya agenda ya Elimu ya Watu Wazima kuwa ya kudumu kwenye mijadala ya elimu kuwa miongoni mwa changamoto zinazorudisha nyuma maendeleo ya Elimu ya Watu Wazimana na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ndani ya Manispaa ya Morogoro.



“Mbali na kujua kusoma, kuhesabu na kuandika, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi hutoa ujuzi na maarifa unaoiua ubora wa maisha kutokana na shughuli na kazi wanazozifanya wawapo kwenye vituo vya kutolea elimu hiyo” alieleza Malimbwi.

Nao wakuu wa Taasisi za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi waliohudhuria katika maadhimisho hayo wameipongeza Serikali kwa kuanzisha Elimu hii kwani imefungua mlango kwa watoto na watu wazima waliokosa elimu ya mfumo rasmi kuweza kupata elimu na kutimiza ndoto zao kimasomo sambamba na kujipatia ujuzi na maarifa muhimu katika maisha yao.



Maadhimisho ya Kilele cha Juma la Elimu ya Watu Wazima Manispaa ya Morogoro yamehudhuriwa na wadau mbalimbali wa elimu wakiwemo Ngunya, WAMO, Mteule na kituo cha mafunzo Stadi Msamvu.

MWISHO